SIGNAL Publishers
Igniting thinking

# DARASA LA NANE

# SIGNAL EXAMS 2022

**THE SCHOLAR**
**002**

## SEHEMU YA KWANZA:
## KISWAHILI - LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

__1__ wa watu nchini kwa jumla hutegemea ujirani mzuri wa watu katika mitaa au vijiji __2__. Hali hii __3__ kabisa mashambani kutokana na raia kuishi pamoja kwa muda mrefu. Kuombana chumvi, __4__ za viberiti na hata __5__ hali ni jambo la kawaida huko. __6__, hali ya mijini ni kinyume kabisa. Ni muhali kupata ushirikiano wa dhati na kweli __7__ majirani. Karibu kila mtu huhiari kuishi kivyake bila bughudha za majirani. Apatwapo na shida ndipo anapogundua kuwa kumbe __8__. Jamaa wake huwa hawapo karibu kuweza kumpiga jeki.

1. A. Maridhiano na utengano B. Mshikamano na utangamano C. Umoja na utengano D. Usuhuba na makabiliano
2. A. viishivyo B. waishimo C. waishivyo D. waishio
3. A. imepuuzwa B. imedunishwa C. imedidimizwa D. imeimarishwa
4. A. njiti B. miti C. vijiti D. moto
5. A. kujuana B. kujulia C. kujua D. kujuliana
6. A. Hata hivyo B. Halikadhalika C. Isitoshe D. Basi
7. A. baadhi ya B. katika C. miongoni mwa D. kati ya
8. A. upweke ni uvundo B. ndugu mui hi kuwa naye C. akufaaye kwa dhiki ndiye raiki D. yajapo yapokee

Nanga ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza katika milki ya Urawa __9__ ili kuamuliwa daawa kwa tuhuma za matumizi __10__ ya mali ya umma. Kiongozi wa Urawa, __11__ Hashibu, alipoingia madarakani aliapa __12__ mizizi yote ya ubadhirifu serikalini. Viongozi wote __13__ walikuwa wameingiwa na tumbojoto kwa wimbi lililokuwa likipiga mbele yao. Idadi ya wale waliojiuzulu __14__. Mashtaka hayo yalikuwa tu mwanzo wa ngoma ambao ni __15__; walivyosema wahenga.

9. A. kusimama kizimbani B. kula kitanzi C. kulishwa kalenda D. kutekwa nyara
10. A. mbaya B. mibaya C. vibaya D. mabaya
11. A. Mfalme B. Diwani C. Rais D. Siti
12. A. kuyang'oa B. kung'oa C. kuing'oa D. kuzing'oa
13. A. wafisidi B. fisadi C. wafisadi D. mifisadi
14. A. waliongezeka B. ziliongezeka C. aliongezeka D. iliongezeka
15. A. sauti B. lele C. mkwiro D. ngozi

***Kutoka swali 16 - 30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo.***

16. **Chagua kiunganishi kifaacho kuunganisha sentensi hizi.**
   Mtaenda nyumbani. Hamna budi kukamilisha zoezi.
   A. Hamna budi kwenda nyumbani kwa kukamilisha zoezi.
   B. Maadamu mmekamilisha zoezi mtaenda nyumbani.
   C. Mtaenda nyumbani na hamna budi kukamilisha zoezi.
   D. Mtaenda nyumbani endapo mtakamilisha zoezi.

17. Teua sentensi iliyotumia kielezi takriri.
   A. Maembe yanayouzwa yaliivishwa kijanja.
   B. Shehe aliyatoa maelezo kwa utaratibu mno.
   C. Waliandikishwa barua wanguwangu.
   D. Mshukiwa aliadhibiwa bure bilashi.

18. Neno '**Tumempa**' lina viambishi vingapi?
   A. 6 B. 7
   C. 3 D. 4

19. Ni orodha ipi iliyo na vivumishi visivyochukua viambishingeli pekee?
   A. Bora, safi, nane, hodari.
   B. Sana, thabiti, mbona, bingwa.
   C. Dhaifu, laini, fisadi, ghali.
   D. Kamili, lini, mwenye, safi.

© Signal Publishers Limited 2022

Website: www. signalpublishers.com. Email. info@signalpublishers.com

SignalPublishers @SignalPublishers

20. Chagua maelezo sahihi.
   A. Sarteni imepakana na Kausi na Zohali.
   B. Zaibaki ndiyo sayari yenye joto jingi zaidi.
   C. Sarteni imezungukwa na pete tatu
   D. Kausi ndiyo sayari iliyodumaa.
21. Ni sentensi ipi iliyotumia kihisishi kwa usahihi?
   A. Aka! Tumefika salama salimini.
   B. Huree! Timu yetu imeshindwa.
   C. Habedari! Mpagazi anakuja na rukwama.
   D. Ebo! Amejifungua mtoto mzuri ajabu.
22. Methali inayowanasihi watu wasijishughulishe na mambo yasiyowezekena ni
   A. kiingiacho mjini si haramu
   B. konzi ya maji haifumbatiki
   C. usisafirie nyota ya mwenzio
   D. dunia mwendo wa ngisi.
23. Bainisha neno lililo tofauti na mengine.
   A. Vipuri B. Chenezo
   C. Dohani D. Fuawe.
24. Chagua sentensi yenye '**ka**' ya kuonyesha kukamilika kwa jambo.
   A. Mti ulikatwa ukaanguka barabarani.
   B. Ka! ondoka hapa sasa.
   C. Kamwite mtoto yeyote nimtume.
   D. Nguo nzito zimefulika zote.
25. Ni jibu lipi lililo sahihi kuhusu alama ya **kitone**, **kihisi** na **kiulizi**?
   A. Zinaweza kutumika katika usemi taarifa.
   B. Huitwa alama za tamatisho.
   C. Zinaweza kutumiwa kukamilisha sentensi.
   D. Hudhihirisha hisia fulani katika sentensi.
26. Ofisi ya mwalimu **mkuu ni tanuri**. Hii ni kumaanisha
   A. ina joto jingi
   B. imejitenga mbali na nyingine
   C. ina mateso mengi
   D. haikubaliwi kuingiwa huko.
27. **Chagua kivumishi kimilikishi katika sentensi ifuatayo.**
   Mkulima aliurudisha uteo wa jirani akauchukua wake mwenyewe.
   A. atauchukua B. wa jirani
   C. wake D. mwenyewe
28. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
   Angani hujifaragua ardhini hujikunyata.
   A. Mbingu na ardhi B. Mwavuli
   C. Mvua D. Ukungu
29. **Andika wingi wa;**
   Mradi wake umeleta uhusiano mwema kijijini hapo.
   A. Miradi yao imeleta uhusiano mwema vijijini hapo.
   B. Miradi yake yameleta mahusiano mema vijijini hapo.
   C. Miradi yao imeleta mahusiano mema vijijini hapo.
   D. Miradi yao yameleta uhusiano mwema vijijini hapo.
30. Chagua mpangilio sahihi.
   A. Herufi → silabi → neno
   B. Silabi → herufi → neno
   C. Neno → herufi → silabi
   D. Herufi → neno → silabi.

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.</u>***

Wingu jeusi tititi liligubika nchi habari zilipotolewa rasmi kuwa rais wa tatu tangu uhuru ulipochukuliwa kwa wakoloni, mstaafu Mwai Kibaki, ametangulia mbele ya haki. Hivyo ilikuwa miaka miwili baada ya mtangulizi wake kufuata njia iyo hiyo. Kama desturi, serikali ilitangaza siku tatu za maombolezo kwa kuwaruhusu raia kuutazama mwili wake katika majengo ya baraza kuu la kitaifa. Siku ya mwisho ya wiki hiyo ilitangazwa kuwa sikukuu ya misa yake. Sifa mzomzo kumhusu zilitolewa na kila aliyepata nafasi ya kuwa jukwaani. Mazishi yake hatimaye yalifanyika kesho yake.

Sifa hizo zote zilitokana na juhudi za mwendazake za kupigania demokrasia pamoja na uongozi wake usioweza kumithilishwa na yeyote katika uongozi wa nchi yetu. Alipochukua hatamu za uongozi mnano mwaka wa 2002, sekta mbalimbali za serikali ambazo zilikuwa zimekwama au zikiyumbayumba ziliimarika. Elimu, uchukuzi, matibabu, zaraa na nyingine zilihitaji uzinduzi na ukarabati mpya. Matumaini ya wakenya yalikuwa juu kuliko wakati wowote tangu mabeberu walipoondoka.

Elimu ya bure kwa wote ni suala ambalo ungetaja kabla ya Hayati Kibaki ungeonekana kukosa urazini. Hata wengi walitilia shaka wakati timu yake ilipokuwa ikipiga kampeni na kulisisitizia. Hayawi hayawi hatimaye yakawa. Katika hotuba yake ya kwanza, alitangaza kuondolewa kwa ada ya shuleni, kuahidi kununua vitabu pamoja na madaftari na hata kalamu. Nyuso za wazazi wengi wasiojimudu kiuchumi ziliteremea kwa bashasha. Hatua hiyo ilipelekea shule kufurika watoto waliokuwa na uchu wa elimu ila wakahiniwa na jinamizi la uchochole. Kiwango cha kujua kusoma na kuandika miongoni mwa raia bila shaka kingepanda na kuwa miongoni mwa nchi bora zaidi barani. Nao wananchi wakielimika kiwango cha maendeleo hakisiti kupaa na kutopea.

Sekta ya uchukuzi ilikuwa imetawaliwa na watu ambao walijawa na uroho na umero wa pesa badala ya thamani ya maisha na uhai. Kuanzia kwa uongozi wa wizara husika hadi kwa madereva na utingo wao, hakuna aliyejali usalama wa **<u>abiria ambao pia si kwamba hawakufaa kuelekezewa lawama</u>**. Serikali yake Rais mstaafu ilileta mabadiliko makubwa kwa sheria ambazo zilileta urazini barabarani. Matwana zilifaa kupakwa rangi maalum na kuwekewa vidhibitimwendo pamoja na mikanda ya usalama. Utingo na maderva waliamuriwa kuvaa sare za kazi huku umma nao ukihamasishwa kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria barabarani. Ajali zilipungua na usafiri ukawa wa kufurahiwa na wote.

Serikali ya Hayati Emilio vilevile ilistawisha na kufufua viwanda mbalimbali vilivyokuwa karibu kuanguka na vilivyoanguka mtawalia. Kiwanda cha maziwa cha K.C.C na K.M.C cha nyama ni baadhi ya vile vilivyoanzisha shughuli baada ya miaka mingi. Ajira zilipatikana kwa vijana na wakulima wakalipwa vizuri kwa jasho lao.

Kutokana na sera muhimu za kiuchumi, nchi ilipiga hatua kubwa kimaendeleo. Maisha ya raia yaliimarika na watu wakawa wanaishi kwa kuchapa kazi kwa bidii iliyoshadidiwa na kaulimbiu ya Rais Kibaki ya 'KAZI

IENDELEE'. Uzalendo nao ulikuzwa kwa ile ya 'NAJIVUNIA KUWA MKENYA.' Mradi kila mmoja akawa anaupiga jeki uongozi katika katika kuukweza uchumi.

Huenda Rais mstaafu Hayati Stanley Emilio Mwai Kibaki ameondoka lakini matendo, sera, mikakati, harakati na sifa alizoacha zitaishi milele. Hata kama hayakuwa mapenzi yake, mojawapo ya barabara kuu, chuo au jengo linaweza kupewa jina la mzalendo huyu ambaye hakutaka kuwa na ubinafsi wowote.

31. Kulingana na aya ya kwanza, ni sahihi kusema
   A. hayati Kibaki alizikwa siku ya Jumamosi
   B. mtangulizi wa mwendazake Kibaki aliendа jongomeo miaka miwili iliyopita
   C. mwili wa marehemu uliwekwa kwenye maeneo ya bunge kwa kutazamwa na wananchi.
   D. hotuba mbalimbali zilitolewa katika misa.

32. Mambo yaliyomzolea Rais Kibaki sifa ni
   A. elimu bora na ya bure, urazini barabarani
   B. kupigana na demokrasia, uongozi mzuri
   C. ushindi, uzoefu katika uongozi
   D. uongozi bora, kuimarisha demokrasia.

33. Mtu angeonekana punguani kwa kutaja elimu ya bure kwa kuwa
   A. kutekelezwa kwake kulionekana kuwa muhali
   B. wananchi wengi walikuwa wamelipuuza
   C. lilikuwa jambo lisilowezekana kamwe
   D. taifa halikuwa na rasilimali za kutekeleza.

34. Waliokumbatia zaidi elimu ya bure ni
   A. wafuasi wa rais
   B. walalahoi
   C. wazalendo
   D. mabwanyenye.

35. Habari hii imedokeza kuwa jambo lililokuwa la kawaida kwa serikali mauti ya rais yatokapo ni
   A. kuenda mazishi ya kijeshi
   B. kuhimiza raia kutoa heshima za mwisho
   C. kutoa habari za tanzia kwa umma
   D. kuidhinisha siku tatu za maombolezo.

36. Yakini wamiliki wa magari walishurutishwa kuweka mikanda ya usalama magarini kwa lengo la
   A. kudhihirisha uzalendo kwa nchi
   B. kupunguza madhara kwa abiria ajali itokapo
   C. kuudhibiti mwendo wa gari
   D. kupunguza na kuzuia ajali barabarani.

37. "**... abiria ambao pia si kwamba hawakufaa kuelekezewa lawama.**" Maneno haya yanamaanisha kuwa abiria
   A. walichangia kulemaza sekta ya usafiri
   B. hawakufaa kulaumiwa kwa lolote
   C. hawakulaumiwa kama washikadau wengine
   D. hawakuwa na makosa yoyote.

38. Kwa mujibu wa aya ya tano, viwanda vilivyokaribia kuanguka
   A. vilianzishwa upya
   B. vilistawishwa na kufufuliwa
   C. vilistawishwa
   D. vilifufuliwa.

39. Kulingana na makala haya, ni kweli kusema kuwa
   A. maisha yamekuwa ghali baada ya kifo cha Rais Mwai
   B. serikali ya Hayati Kibaki haikuwa na visa vya ufisadi
   C. uongozi wa Hayati Emilio ndio bora tangu uhuru
   D. elimu ya bure imewawezesha vijana wote kupata ajira.

40. Pendekezo la mwandishi ni kuwa
   A. sehemu muhimu kama baraste zinaweza kupewa jina la mwendazake kama kumbukumbu
   B. taalimbiu za mwendazake zifundishwe shuleni ili kukuza uzalendo
   C. mwendazake hakupendelea jina lake kupewa sehemu mbalimbali nchini
   D. watu wote waepuke ubinafsi kama alivyokuwa mwendazake.

***__Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.__***

Hayawi hayawi huwa. Zimwi lililoutikisa ulimwengu mzima-jambo ambalo halijawahi kutokea katika kizazi hiki au hata cha jana lilitangazwa kuishiwa nguvu rasmi. Sheria kalikali za kujikinga kama vile kuvaa barakoa na kunawa kila mara, zilisitishwa. waliokuwa na **__kismati__** kuliepuka walirejelea shughuli zao japo kwa majonzi ya kufiwa na jamaa au rafiki yao kutokana na korona.

Idadi ya vifo vilivyotangazwa katika bara letu ilikuwa tu kama miale ya moto ikilinganishwa na mabara mengine yaliyofikiwa na moto wenyewe halisi. Kwa hivyo tangazo lilipotolewa watu walishusha pumzi na kupiga dua.

Miongoni mwa shughuli zilizorejelewa ni kufunguliwa kwa shule na vyuo nchini. Kwa Sirini, tangazo hilo lilikuwa kama bomu la atomiki lililoangushwa kichwani mwake. Hakuwa tayari. Lakini angefanyaje? Baba yake aliyekuwa simba alisisitiza umuhimu wa kufika shuleni siku ya kwanza. Hivyo hakuwa na budi ila kujiandaa kwa safari ya keshoye.

Kama kawaida, wasimamizi wa shule waliwaalika wauguzi shuleni kwa shughuli ya kupima ujauzito. Hii ilikuwa kawaida katika shule nyingi nchini. Hatua hii ilichukuliwa ili kuhakikisha kuwa hakuna uavyaji mimba shuleni mbali na kuhakikisha udumishaji wa maadili baina ya wanafunzi. Kama ilivyokuwa desturi, wauguzi

hao walianza na wanafunzi wa kidato cha kwanza. Shughuli yenyewe ingechukua kutwa yote. Waliopatikana kuhimili walipewa ushauri nasaha kisha kutumwa nyumbani huku wakitarajiwa kurudi baada ya kujikopoa.

Zamu ya Sirini ilifika. Alienda kwa ujasiri na ukakamavu kama wasichana wengine. Uchunguzi ulifanywa na akaelekea fefefe kwenye dahalia. Kule walijuliana hali na kusimuliana ya likizo kwa bashasha. Sirini alipokuwa akivipanga vitabu alihisi kitefutefu. Hii ilikuwa mara yake ya tatu sasa. Hakujua sababu wala asili yake. Chenyewe hakikuwa kikidumu zaidi ya dakika chache tu. Kila alipohisi hivyo angesimama na kutulia kwa muda ili kupumua hewa safi aliyoona labda alikosa.

Kesho yake, siku ya matokeo ya uchunguzi, waliingia madarasani. Mara Sirini aliitwa na naibu msimamizi wa masuala ya kijamii shuleni, Bi Tande. Msimamizi alikuwa ndiye mwalimu mkuu. Kuitwa huko kulimtia tumbojoto. Walipofika ofisini, mwalimu alimuuliza maswali mawili matatu kisha akatoa faili yenye karatasi nyingi kisha akaitoa mojawapo ya hizo karatasi.

"Tazama hii Sirini. Hii ni ithibati kuwa hukuwa nyumbani wiki moja baada ya shule kufunguliwa hata kama unakanusha. Kama ungekuwa nyumbani basi hungekuwa na mimba," alisema Bi Tande. Sirini alihisi dunia ikizunguka na kutishia kumwangukia. Akahisi sauti kali kichwani kisha akaanguka sakafuni pu! Giza likatanda.

---

**41.** Sentensi ya kwanza inaashiria
A. kuwepo kwa zimwi hatari ulimwenguni
B. mwanzo wa maisha huru yasiyo na majanga
C. ulimwengu kuishiwa nguvu baada ya janga la korona
D. nafuu ya kuisha kwa janga la korona.

**42.** Maafa ya bara la Afrika yanalinganishwa na miale ya moto kwa sababu
A. athari zake zilipiku zile za mabara mengine
B. halikuchukua tahadhari ifaayo kama mabara mengine
C. watu wengi waliangamia
D. hayakuwa makubwa kama ya kwingine.

**43.** Neno **kismati** limepigiwa mstari. Linamaanisha
A. bahati ya mtende
B. ujasiri
C. utulivu
D. lishe bora.

**44.** Si kweli kwamba
A. Sirini alipokea tangazo kwa hisia mseto
B. Korona ilisitisha masomo nchini
C. Sirini alienda shuleni shingo upande
D. tangazo liliwaletea raia nafuu.

**45.** Uchunguzi uliofanywa kwa banati shuleni ulikuwa na malengo gani?
A. Kunasihi kizazi, kudumisha elimu.
B. Kunasa washerati, kuimarisha jina la shule.
C. Kuokoa ujauzito, kuhimiza hulka nzuri.
D. Kuzuia mimba, kukuza maadili.

**46.** Iwapo mmoja angepatikana na mimba
A. angeonywa vikali na kuruhusiwa kwenda kujifungua kwanza
B. angepewa mawaidha na kuruhusiwa kwenda kujifungua
C. angehitimisha masomo baada ya kupewa maonyo
D. angenasihiwa na kufukuzwa nyumbani.

**47.** Aya ya tano imedhihirisha kuwa
A. Sirini aliifahamu hali yake
B. kichefuchefu kilisababishwa na ukosefu wa hewa safi
C. Sirini alikuwa limbukeni katika kutambua hali ya ujauzito
D. Sirini hakupenda shughuli nzima ya uchunguzi.

**48.** Bi. Tande alikuwa
A. msaidizi wa mwalimu mkuu katika mambo ya kijamii shuleni
B. mwalimu msimamizi wa masuala ya kijamii shuleni
C. naibu wa mwalimu mkuu
D. mwalimu mkuu.

**49.** Kulingana na Bi Tande
A. Sirini alihepa shuleni wiki moja baada ya kufunga
B. Sirini alihimili mwanzoni mwa likizo
C. Sirini alikataa kutambua aliyemringa
D. Sirini alikuwa na mimba ya wiki moja.

**50.** Chagua kauli sahihi kulingana na mwisho wa aya ya mwisho.
A. Uzito wa dunia ulimwua Sirini.
B. Sirini alipoteza fahamu.
C. Ulikuwa usiku giza lilipoingia.
D. Nguvu za umeme zilipota ofisini.